



JUMUIYA YA WANATAALUMA
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (UDASA)
S.L.P. 35091 Dar es Salaam, Tanzania
Barua pepe: udasa@udsm.ac.tz



27 Novemba 2025

Kumb Na. UDASA/2025/ALL/01

**Kwa Wana-UDASA Wote,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

Ndugu Wana-UDASA

Yah: Kutekeleza Maelekezo ya Uongozi wa UDASA Kuhusu Uboreshaji wa Taaluma na Kupata Maslahi Stahiki

Tafadhali rejea kichwa cha barua hii.

1. Kwa niaba ya Uongozi wa UDASA, nimeandika barua mbili kwenda kwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) kumuomba kutekeleza mambo muhimu 2:
 - Kuhakikisha kila kitengo kinakuwa na kituo cha kuchapishia, kurudufishia, na kuskania taarifa mbalimbali zinazohusiana na taaluma ambazo wana-UDASA tunazifanya kila siku.
 - Kuhakikisha malipo yote yanayohusiana na usimamimizi na utahini wa tasnifu za shahada za awali, uzamili na uzamivu yanalipwa kwa wakati.
2. Kwamba, utekelezaji wa mambo haya mawili siyo msaada. Ni matakwa ya lazima kwa mujibu wa kanuni, taratibu na miongozo inayosimamia utekelezaji wa majukumu ya kitaaluma katika chuo chetu.
3. Kwa barua hii nawaelekeza wana-UDASA wote kuhakikisha tunapatiwa stahiki zetu za kitaaluma kwa mujibu wa matakwa ya kitaaluma kama ambavyo barua nilizomwandikia Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) zinaeleza.
4. Endapo maombi haya 2 hayatakuwa yametekelezwa kufikia tarehe 5 January 2026, kila mwana-UDASA ajiandae kwa ajili ya kusitisha huduma ambazo ufanisi wake unategemea utekelezaji wa yale ambayo yamebainishwa kwenye barua husika ambazo nimeziambatanisha.

Wako katika Uhuishaji wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,

Elgidius E.B. Ichumbaki (PhD., H.D. Uni. Bra),
Mwenyekiti na Mtendaju Mkuu wa UDASA.

Nakala:

Makamu Mkuu wa Chuo

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo—Utawala

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo—Utafiti

Mtaa wa Uvumbuzi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35091, Dar es Salaam – Tanzania

Simu: Mwenyekiti UDASA +255 713 860875; Katibu UDASA +255 757 984 595

Barua pepe: ichumbaki@udsm.ac.tz; makukula.dominicus@udsm.ac.tz

Tufuatilie kupitia  [udasaudsm](https://www.facebook.com/udasaudsm)



JUMUIYA YA WANATAALUMA
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (UDASA)
S.L.P. 35091 Dar es Salaam, Tanzania
Barua pepe: udasa@udsm.ac.tz



25 Novemba 2025

Kumb Na. UDASA/2025/DVC-ARC/DPGS/01

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo–Taaluma,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ndugu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo,

**Yah: Kulipa Stahiki za Wana-UDASA Zinazohusiana na Usimamizi wa Mitihani
na Tasnifu za Wanafunzi wa Umahili na Uzamivu**

Tafadhali rejea kichwa cha barua hii.

1. Jumuiya ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDASA) ilianzishwa na inafanya kazi kwa mujibu wa Kifungu cha 48 cha Sheria ya Vyuo Vikuu ya Tanzania (2005) na Kifungu cha 26 cha Hati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam [University of Dar es Salaam Charter] (2007).
2. Kama unavyofahamu, Muhula wa Kwanza wa Mwaka Mpya wa masomo wa 2025/2026 tayari umeanza, na wana-UDASA wanaendelea kutimiza majukumu yao ya kitaaluma.
3. Lakini, kupitia wajumbe wa Kamati Tendaji ya UDASA na wawakilishi wa UDASA walioko kila kitengo husika, imebainika kwamba kwa muda mrefu wana-UDASA wamekuwa wakitekeleza majukumu yao ya kusimamia tasnifu za umahili na uzamivu, na pia kuhudhuria mikutano mahsusi ambapo wanafunzi hufanya utetezi wa tasnifu zao (*viva voce*), bila kulipwa stahili zao (kwa maana posho ya usimamizi, usahihishaji tasnifu na posho ya kikao wakati wa mtihani) kwa wakati.
4. Kutokuwalipa wana-UDASA stahiki zao kwa wakati (kuwakopa) ni kinyume na taratibu na kanuni za usimamizi wa shahada za umahili (2018) na Waraka wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wa mwaka 2024 kuhusu motisha kwa wafanyakazi. Hali hii siyo tu inadhoofisha morali ya wana-UDASA kutekeleza majukumu yao ya kuwasaidia na kuwawezesha wanafunzi kumaliza shule kwa wakati bali pia inawafanya wanataaluma kujenga chuki dhidi ya utawala wa Chuo Kikuu na Serikali ya Tanzania kwa jumla.

5. Katika kutekeleza Kifungu cha 3 cha Katiba ya UDASA ya Mwaka 2016, ninakuandikia kukumbusha wajibu wako wa kuhakikisha wana-UDASA (wanachama wetu) wanapata stahiki zao kila wanapotekeleza majukumu yao ya kusimamia na kutahini tasnifu bila kuchelewa. Kwa barua hii, kukuomba na kukuhimiza kuhakikisha wana-UDASA wanapata stahiki zao kwa wakati. Kama chuo kinaweza kulipa posho za wajumbe wa vikao mbalimbali vya maamuzi, tena muda ule ule wakati kikao kikiwa kinaendelea, inashindikana nini kulipa fedha za walimu wanaotekeleza majukumu yao ya kusahihisha/kutahini tasnifu?
6. Ninaomba na kutoa wito kwako kuhakikisha wana-UDASA wanapata stahiki zao pindi wanapokamilisha kusimamia na kutahini tasnifu. Vile vile, ninatumia fursa hii kukujulisha kuwa, ifikapo Januari 5, 2026, wana-UDASA wote ambao wanashiriki kusimamia, kusahihisha na kutahini tasnifu watasitisha huduma hizi endapo hawatalipwa stahiki zao kwa wakati na kwa mujibu wa taratibu za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nakushukuru kwa kulipa jambo hili uzito unaotakiwa kwa maendeleo ya taaluma na kuboresha utendaji kazi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wako katika Uboreshaji Taaluma,



Elgidius E.B. Ichumbaki (PhD., H.D. Uni. Bra),
Mwenyekiti na Mtendaju Mkuu wa UDASA.

Nakala:

Makamu Mkuu wa Chuo

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo—Utawala

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo—Utafiti

Katibu wa UDASA – Kwa ufuatiliaji

Wana-UDASA wote –Kwa Utekelezaji.



JUMUIYA YA WANATAALUMA
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (UDASA)
S.L.P. 35091 Dar es Salaam, Tanzania
Barua pepe: udasa@udsm.ac.tz



11 Novemba 2025

Kumb Na. UDSM/UDASA/2025/DVC-ARC/01

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Taaluma,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ndugu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo—Taaluma,

**Yah: Kuwezesha Kila Idara Kuwa na Kituo cha Kupata Huduma za Kuchapisha,
Kudurufu na Kuskani Nyaraka Mbalimbali Zinazohusiana na Kazi za Kitaaluma**

Tafadhali rejea kichwa cha barua hii.

1. Jumuiya ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDASA) ilianzishwa na inafanya kazi kwa mujibu wa Kifungu cha 48 cha Sheria ya Vyuo Vikuu ya Tanzania (2005) na Kifungu cha 26 cha Hati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam [University of Dar es Salaam Charter] (2007).
2. Kama unavyofahamu, Muhula wa Kwanza wa Mwaka Mpya wa masomo wa 2025/2026 unaanza, hivyo, kuwataka wana-UDASA kufanya maandalizi stahiki ili kutimiza majukumu yao ya kitaaluma.
3. Lakini, kupitia wajumbe wa Kamati Tendaji ya UDASA na wawakilishi wa UDASA walioko kila kitengo, imebainika kwamba Idara nyingi hazina huduma za kuchapisha (printing), kudurufu/kunakili (photocopying) na kuskani (scanning) ili kuwezesha shughuli nyingi za kitaaluma ikiwepo kufundisha, kusimamia wanafunzi, kuwasiliana na vitengo mbalimbali ndani na nje ya chuo, na hivyo kutekeleza majukumu ya msingi ya kufundisha, kushauri na kutafiti.
4. Ikumbukwe kuwa vifungu vya 10-15 vya Hati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2007) vinawataja ma-Rasi, ma-Amidi na Wakurugenzi kama wasimamizi wa taaluma na utawala katika vitengo vyao. Hii ina maana kwamba, ni wajibu wao kuhakikisha kila idara inakuwa na kituo au ofisi maalum yenye kuwapatia wanataaluma wote huduma hizi muhimu katika kutekeleza majukumu yao ya kitaaluma.
5. Pamoja na UDASA kutambua umuhimu wa kutumia nakala tepe na njia nyinginezo za mawasiliano kidijitali, katika kutekeleza Kifungu cha 3 cha

Mtaa wa Uvumbuzi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35091, Dar es Salaam – Tanzania

Simu: Mwenyekiti UDASA +255 713 860875; Katibu UDASA +255 757 984 595

Barua pepe: ichumbaki@udsm.ac.tz; makukula.dominicus@udsm.ac.tz

Tufuatilie kupitia     [udasaudsm](https://www.facebook.com/udasaudsm)

Katiba ya UDASA ya Mwaka 2016, ninakuandikia kukuomba uwakumbushe na uwatake ma-Rasi, ma-Amidi na Wakurugenzi kutekeleza wajibu wao wa kuhakikisha wana-UDASA (wanachama wetu) wanapata huduma hizi muhimu. Kwa barua hii ninakuomba na kukuhimiza kuhakikisha huduma nilizozitaja zinapatikana katika vitengo husika haraka iwezekanavyo.

6. Kwa mamlaka yako kama Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anayesimamia taaluma, ninakuomba pia uwe tayari kuchukua hatua za kinidhamu endapo upatikanaji wa huduma hizi hautapewa kipaombele kwa kila Idara. Aidha, kwa kipindi hiki ambacho Ndaki, Shule Kuu na Kurugenzi zinajipanga kutekeleza ombi hili, tutawashauri wana-UDASA kutumia ofisi za ma-Rasi, ma-Amidi na Wakurugenzi wa vitengo wanakofanya kazi.

Natanguliza shukurani kwako binafsi na ofisi yako pia kwa kuona umuhimu wa ombi langu na kulipa uzito unaostahili ili kutimiza matakwa ya msingi ya kuboresha utendaji kazi wa wanataaluma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wako katika Uboreshaji Taaluma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,



Prof. Elgidius E.B. Ichumbaki (PhD., H.D. Uni. Bra),
Mwenyekiti na Mtendaju Mkuu wa UDASA.

Nakala:

Makamu Mkuu wa Chuo—Taaluma,

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo—Utawala

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo—Utafiti

Katibu wa UDASA – Kwa ufuatiliaji

Wana-UDASA wote –Kutoa mrejesho juu ya upatikanaji wa huduma tajwa.